

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA  
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**621**


**KISWAHILI**

**Muda: Saa 3**

**Mwaka : 2021**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A, maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu B na C.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B na C zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



2

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Eleza kwa kifupi tanzu nne za Fasihi Simulizi.
2. Eleza kwa kifupi jinsi stadi za kuandika na za kuzungumza zinavyotofautiana katika vipengele vifuatavyo:
  - (a) Kiwakilishi
  - (b) Kikomo
  - (c) Uhusiano
  - (d) Suluhisho
3. Andika sentensi zifuatazo katika kauli ya kutenda:
  - (a) Mpira umechezwa na mtoto.
  - (b) Kazi yote imemalizwa na fundi.
  - (c) Wezi wamepigwa na askari.
  - (d) Nguo zimekaushwa na mimi.
  - (e) Watoto wamepigwa na mama yao.
  - (f) Mpira umeingizwa vizuri na mfungaji.
  - (g) Kuku wa baba ameliwa na mbwa wa jirani.
  - (h) Juma ameitwa na rafiki yake.
4.
  - (a) Eleza kwa kifupi dhana ya kusoma kwa ziada.
  - (b) Taja hatua nne za kusoma kwa ziada.
5. Eleza maana ya dhana zifuatazo:
  - (a) Shairi
  - (b) Ngonjera
  - (c) Utenzi
  - (d) Kina
6. Bainisha shughuli nne za wanafunzi wakati mwalimu anawasilisha maudhui ya somo katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.
7. Ni mambo gani atakayoyazingatia mwanafunzi wakati wa uandishi wa insha? Taja manne.
8. "Masimulizi ni mbinu bora ya kufundishia mada ya fasihi katika shule za msingi." Fafanua kwa kifupi faida nne za kutumia mbinu hiyo.
9. Orodhesha mambo manne ya kuzingatia ili kupata ujumbe katika habari inayosikilizwa au inayosomwa.
10. Eleza kwa muhtasari hasara nne za kutokutumia zana za kufundishia na kujifunzia wakati wa ufundishaji.

### SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili** (2) kutoka sehemu hii.

11. Kwa kutumia mfano kwa kila moja, eleza sifa nne za fasihi simulizi.
12. "Lugha ni chombo muhimu cha mawasiliano katika jamii." Tetea kauli hii kwa kutumia hoja tano.
13. Kwa kutumia mfano, eleza matumizi matatu kwa kila alama za uandishi zifuatazo kama zinavyotumika katika uandishi.
  - (a) Nukta (.)
  - (b) Mkato (,)
  - (c) Alama ya kuuliza (?)
  - (d) Nukta na mkato (;)
  - (e) Mshangao (!)

### SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili** (2) kutoka sehemu hii.

14. Kwa kutumia mifano, fafania namna nne na faida mbili za kuhifadhi zana za kufundishia na kujifunzia.
15. Fafania faida sita za alama za majaribio katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.
16. Kwa kutumia hoja sita, eleza jinsi utakavyofundisha nomino na vivumishi kwa wanafunzi wa Darasa la Sita.